



Kielelezo cha Kuripoti Tukio la UEMS

Milipuko isiyotarajiwa katika maeneo ya kuhifadhi zana za kivita (*Unplanned Explosions at Munitions Sites - UEMS*) ni jambo muhimu la kiusalama kwa serikali na ni changamoto kubwa ya usalama kwa jamii ya kimataifa. Utafiti huu wa Silaha ndogo ndogo umerekodi zaidi ya matukio 500 kama hayo kwa kipindi cha miaka 35, kuanzia 1979 hadi 2013. Uchambuzi wa takwimu hizi unaonekana katika Kijitabu kilichotoka kutoka kiitwacho “Unplanned Explosions at Munitions Sites: Excess Stockpiles as Liabilities rather than Assets” kilicho na majedwali, michoro, ramani, na viambatisho vingine muhimu, mlundikano mkubwa wa silaha hauna umuhimu wowote na sio Rasilimali.¹ Milipuko inayotokana na silaha hizi imetokea katika nchi 100 (angalia Ramani 1), na imesababisha vifo vya maelfu ya watu, maelfu ya watu kujeruhiwa, watu kukimbia makazi, mamilioni ya fedha za kigeni kutumika katika gharama za usafirishaji, kutegua mabaki ya mabomu, kununua silaha zingine na kufidia zilizolipuka. Rasilimali hizo zingeweza kutumika kwa namna nyingine yenye manufaa zaidi. Baadhi ya matukio ya milipuko yamesababisha mawaziri wa serikali, maofisa wa kiraia, na maafisa wa kijeshi kukamatwa na kuondolewa madarakani.

Kielelezo cha UEMS inazungumzia kuhusu tatizo kubwa zaidi la uharibifu unaosababishwa na mlipuko mmoja. Matukio yanaonyesha fikra zisizo furahisha za watunga sera kuhusu viwango vinavyofaa vya akiba na viwango hatari vya ziada. Matukio mengi hutokea kwa sababu mataifa mengi huchukulia akiba zao za zana za kivita kama rasilimali badala ya madhara, bila kujali muda gani zimehifadhiwa na jinsi zilivyohifadhiwa.

Kutambua na kuteketeza akiba ya ziada kunafaa kuwa hatua muhimu ya mara kwa mara kwa ajili ya usimamizi mzuri wa silaha. Wakati silaha zinawekwa bila kujali kiwango, ubora, na usalama wa hifadhi, usimamizi

unapungua. Katika hali kama hiyo, huwa kuna uwezekano wa uhamishaji silaha wenye utata na uwezekano wa kubadilisha matumizi kwa bahati mbaya au bila idhini.

Kijitabu hiki kinatumwa kwa sababu tatu za msingi. Ya kwanza, kinalenga kusaidia utendaji bora kwa kufafanua ukubwa na uwezo wa changamoto ambayo watunga sera hupitia, na kinahamasisha mataifa kusimamia akiba zao za silaha ndogo kwa ufanisi. Ya pili, utafiti unakusudiwa kutumiwa kama zana ya dondoo. Kwa mfano, hali halisi inaonekana kwa mataifa 37 yanayotekeleza shughuli zinazohusiana na UEMS (angalia Mchoro 2). Na ya tatu, kitabu hiki kinatumwa kama zana ya mafunzo.


Kielelezo cha Kuripoti Tukio

Kielelezo cha Kuripoti Tukio la UEMS (*UEMS Incident Reporting Template - UEMS IRT*) (angalia Mchoro 1) kinatolewa ili kusaidia uwekaji wa rekodi sahihi na kushiriki takwimu zilizo kwenye mfumo.

Taarifa sahihi kwenye kila tukio la UEMS zinahitajika ili kuboresha jitihada za uzuiaji wa matumizi ya silaha ndogo. Uchambuzi wa takwimu za majanga yanayotokana na matumizi ya silaha ndogo duniani unatoa michango miwili muhimu. Umuhimu wa kwanza: Kuongezeka kwa ufahamu wa marudio ya matukio haya kunaweza kupunguza madhara yanayohusiana na mlipuko na hatimaye, inafaa kuhamasisha mamlaka husika kuboresha utendaji wao hususan usalama wao wa kimwili na usimamizi wa akiba ya silaha (*Physical Security and Stockpile Management - PSSM*). Umuhimu wa pili: Uchambuzi wa takwimu za kimataifa unaweza kudhihirisha mitindo au mbinu mbalimbali zinazotumika katika matukio ya UEMS, jambo ambalo linaweza kuboresha uwezo wa kutambua hali hizo ambazo zinaweza kuongeza idadi ya matukio.

Katika miaka 35 iliyopita, vyombo vya habari havijaweza kutoa taarifa zilizofanyiwa utafiti wa kina kwa jamii badala yake wanatoa maoni na uvumi wa mwanzo kuhusu sababu za tukio na sio taarifa kamili. Vyombo vya habari vinalenga kutoa taarifa za vifo, uharibifu wa mali au miundombinu. Taarifa kamili hupatikana baada ya upelelezi na kwa kawaida taarifa hizo hutolewa kwa umma kwa nadra.

Kwa kawaida serikali husita kutoa taarifa za uchunguzi. Kuthibitisha hili, kwa mfano, wanaweza wasitoe taarifa kwa sababu za



Mchoro 1. Kielelezo cha Kuripoti Tukio la UEMS

1. Lini? (Tuko la UEMS lilitokea lini?)

Tarehe (mmmm/mm/ss): / /

Saa (ss:dd) [kwa mfumowa saa 24]: :

Hali ya hewa (k.m. kiasi cha joto °C, upepo, mvua, radi):

2. Wapi? (Tukio la UEMS lilitokea wapi?)

Nchi:

Jiji au mji:

Jina la kituo/eneo:

3. Nani? (Ni nani anayemiliki au kusimamia eneo na vitu vilivyomo?)

3.1. Ni nani anayemiliki au kusimamia eneo?

Miliki	<input type="checkbox"/> taifa	<input type="checkbox"/> sio taifa
	msimamizi (kama ni tofauti)	
Maelezo (k.m. aina)	<input type="checkbox"/> polisi	<input type="checkbox"/> jeshi
	<input type="checkbox"/> kigeni (k.m. kikosi cha kudumisha amani)	<input type="checkbox"/> kampuni binafisi
	<input type="checkbox"/> wengine (k.m. makampuni ya kitaifa), taja:	<input type="checkbox"/> kundi lenye silaha
	<input type="checkbox"/> wengine (k.m. makampuni ya kitaifa), taja:	<input type="checkbox"/> wengine (k.m. genge la jinai), taja:

3.2. Zana hizo za kivita zinawekwa katika jengo la aina gani?

3.2.1. Hali ya eneo la hifadhi?	<input type="checkbox"/> la kudumu	<input type="checkbox"/> la muda
3.2.2. Ni shughuli za aina gani zilizofanyika hapo?	<input type="checkbox"/> kuhifadhi	
	<input type="checkbox"/> kuchakata	
	<input type="checkbox"/> kupakia/kupakua	
3.2.3. Muundo wa jengo la hifadhi ulikuwaje?	<input type="checkbox"/> jengo lililojengwa kwa madhumuni ya hifadhi	
	<input type="checkbox"/> jengo lililojengwa kwa madhumuni mengine mbali na hifadhi	
	<input type="checkbox"/> ghala	
	<input type="checkbox"/> haijulikani	

3.3. Ni zana zipi za kivita zilihifadhiwa hapo?

Maoni (k.m. umri, asili, aina, na hali ya zana za kivita)	<input type="checkbox"/> ndege	<input type="checkbox"/> vifaru na mizinga
	<input type="checkbox"/> mkusanyiko wa silaha mbalimbali	<input type="checkbox"/> milipuko na baruti
	<input type="checkbox"/> mabomu ya kutega ardhini	<input type="checkbox"/> silaha za majini
	<input type="checkbox"/> silaha ndogondogo na nyepesi	<input type="checkbox"/> haijulikani
Aina ya nyenzo au zana za kivita:		Kiwango/kipimo (makadirio ya jumla, yanayotoa takwimu yoyote inayopatikana):
		<input type="checkbox"/> kiwango (kwa idadi)
		<input type="checkbox"/> uzito (kwa tani)
		<input type="checkbox"/> thamani (onyesha kwa fedha)

4. Kwa nini? (Kwa nini tukio la UEMS lilitokea?)

(k.m. uharibifu wa zana za kivita; uhifadhi mbaya au miundombinu mibovu; nyenzo kutumiwa vibaya au kuangushwa; matukio ya nje kimazingira (kama vile mafuriko au moto); usalama mdogo; mazingira mabaya ya kufanyia kazi)

5. Nini? (Ni nini kilichotokea kama matokeo ya mlipuko?)

5.1. Eneo lililoathiriwa ni kubwa kiasi gani?	5.2. Ni nani aliathiriwa na mlipuko?	5.3. Ni miundombinu gani iliharibiwa na mlipuko?:
Nusu kipenyo cha mlipuko (km) <input type="text"/>	Vifo (jumla) <input type="checkbox"/> ndiyo <input type="checkbox"/> hapana <input type="checkbox"/> haijulikani	Aina ya miundomsiingi iliyoharibiwa (chagua yote inayohusika)
(ukubwa wa shinikizo la hewa/mgandamizo wa hewa kutoka eneo la mlipuko)	Kama ni ndiyo, idadi ya wafanyakazi katika eneo hilo waliokufa <input type="text"/>	<input type="checkbox"/> shule
	idadi ya raia, watu waliokufa wasio wafanyakazi <input type="text"/>	<input type="checkbox"/> makazi
Nusukipenyo cha usaambaaji wa hewa ya mabomu (km) <input type="text"/>	Majeruhi (jumla) <input type="checkbox"/> ndiyo <input type="checkbox"/> hapana <input type="checkbox"/> haijulikani	<input type="checkbox"/> huduma za afya
(ukubwa wa eneo lililoathiriwa na risasi, mlipuko, silaha, na vifus/mabaki, vinavyosababisha hatari endelevu)	Kama ni ndiyo, idadi ya wafanyakazi wa eneo hilo waliojeruhiwa <input type="text"/>	<input type="checkbox"/> kitovu cha usafiri
	idadi ya raia, wasio wafanyakazi waliojeruhiwa <input type="text"/>	<input type="checkbox"/> mingine, taja: <input type="text"/>
Maoni <input type="text"/>		Kiwango cha uharibifu (andika fedha) <input type="text"/>

5.4. Matokeo mengine ya UEMS ni yapi?


Jibu la serikali	Fidia <input type="checkbox"/> ndiyo <input type="checkbox"/> hapana <input type="checkbox"/> haitumiki	Kama ni ndiyo, ni familia ngapi zilipokea fidia? <input type="text"/>
<input type="checkbox"/> uchunguzi wa kiusalama		
<input type="checkbox"/> uchunguzi wa kisheria		
Matokeo ya kisiasa (k.m. maafisa wakuu kukaripwiwa, kushushwa vyeo, kutuhumiwa, au kufungwa jela)	Matokeo mengine (k.m. ya kimazingira, kiuchumi, kijamii, au kiafya)	

6. Vipi? (Je, Taifa na jamii ya kimataifa ilisemaje?)

Mpango wa hatua za dharura ulitekelezwa?	Mtaalamu wa EOD* alikuwa katika eneo kabla?	Uhamishaji wa wakimbizi Kama ni ndiyo, watu wangapi? <input type="text"/>	Mtoa taarifa, maelezo ya mawasiliano
<input type="checkbox"/> ndiyo <input type="checkbox"/> hapana <input type="checkbox"/> haitumiki	<input type="checkbox"/> ndiyo <input type="checkbox"/> hapana <input type="checkbox"/> haijulikani	<input type="checkbox"/> ndiyo <input type="checkbox"/> hapana <input type="checkbox"/> haitumiki	Jina <input type="text"/>
Watu waliohamishwa Kama ni ndiyo, watu wangapi? <input type="text"/>	Uondolewaji wa UXO** <input type="checkbox"/> ndiyo <input type="checkbox"/> hapana <input type="checkbox"/> haitumiki	Maelezo (k.m. wingi au uzani kwa tani) <input type="text"/>	Taasisi <input type="text"/>
Kama ni ndiyo, uhamishaji ulikuwa wa muda au <input type="checkbox"/> wa kudumu?			Anwani ya posta <input type="text"/>
Maoni (k.m. majina ya washiriki wanaosaidia, ikijumuisha washiriki wa ndani, kitaifa, au kimataifa)			Simu <input type="text"/>
			Barua pepe <input type="text"/>

*Explosive ordnance disposal / Kanuni za kuharibu Mizinga na Mabomu; **Unexploded ordnance.

Ramani 1. Matukio ya UEMS kwa nchi, 1979-2013



kusalama hasa wanapotoa taarifa muhimu zinazohusu hifadhi za zana za kivita au vikwazo vya kisheria vinavyowakumba watu binafsi au taasisi kama sababu za kuzuia utoaji sahihi wa taarifa.

UEMS IRT imeundwa kuweka viwango na kuhamasisha ukusanyaji wa taarifa za matukio kama hayo. Muundo mzuri wa UEMS IRT unapunguza wasiwasi ambao mataifa yamekuwa nao na unawasaidia wanahabari kutambua vipengele zaidi vinavyotakiwa kuhusu matukio ya UEMS.

Kielelezo kinawawezesha watu wasio wataalamu kutoa taarifa vizuri zaidi. kwa faida zaidi, kielelezo kizuri kinawezesha mamlaka kuwasilisha muhtasari kamili kuhusu tukio, bila kutoa taarifa kamili za uchunguzi kwa ukamilifu wake.

Uchunguzi

Athari za UEMS ni kubwa na maran-yingi huwa za muda mrefu. Vyombo vya habari hulenga athari za mwanzo za tukio, kama vile vifo na majeruhi waliopatikana kutokana na mlipuko wa awali. Hii inalengavifo na majeruhi;

ni kiashirio muhimu cha gharama za UEMS na ndiyo maana ni muhimu kutafuta njia za kuzuia. Ni wakati tunapoangalia madhara ya muda mrefu ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kijeshi, hata hivyo, kuna uwezekano wa kuelewa gharama kamili ya UEMS na kwa nini kukumbana nazo kunafaa kupewa kipaumbele katika ajenda za kitaifa, kikanda na kimataifa. Hadi leo, UEMS IRT imeundwa kusaidia kutoa unasaji mzuri wa takwimu na uwekaji mzuri wa kumbukumbu. ■

Vidokezo

- 1 Muhtasari 6, 'Milipuko isiyotarajiwa katika maeneo ya kuhifadhi zana za kivita,' unaopatikana kwa lugha mbalimbali, unatoa ufupisho.

Vyanzo

Muhtasari huu wa Utafiti umetengenezwa kulingana na toleo la mfululizo la Kijitabu cha Small Arms Survey la "Unplanned Explosions at Munitions Sites (UEMS): Excess Stockpiles as Liabilities rather than Assets", lililohaririwa na Eric G. Berman na Pilar Reina.

Mchoro 2. Wasifu wa sampuli : Mhusika anayetekeleza au kutoa shughuli na huduma zinazohusiana na UEMS*

HANDBOOK

Unplanned Explosions at Munitions Sites

Multinational Small Arms and Ammunition Group (MSAG)

HEADQUARTERS
n/a

WEBSITE
www.msag.es

POC
NAME n/a
TITLE n/a
msag@msag.es
n/a

SHORT DESCRIPTION
MSAG, established in 2005, is an apolitical, informal, and multinational platform which strives to develop training modules, support standard setting, share experience, and coordinate assistance concerning PSSM. Its 15 members contribute according to national priorities and capacities.

UEMS-RELATED ACTIVITIES
MSAG was created to assess how international instruments promoting stockpile management could be implemented effectively. MSAG contributes to standard-setting efforts, develops training modules for donor nations, implements common projects, and provides a platform to exchange knowledge and expertise. MSAG offers classroom- and field-based training to decision-makers, practitioners, and managers. MSAG nations can provide comprehensive support in the establishment of proper life-cycle management of weapons and munitions. MSAG's half-yearly meetings (the 18th was held in November 2013) improve coordination, facilitate pooling of resources, and help to prevent costly duplication of efforts. (These meetings benefit from expertise from international and regional institutions as well as from civil society organizations.) A typical project cycle for a country receiving assistance from MSAG would include an assessment visit, awareness raising, project planning, training and technical advice, supporting implementation, and reassessment and evaluation of changing needs and progress made.

ADHERENTS TO COMMITMENTS AND RECIPIENTS OF ASSISTANCE
MSAG members (Austria, Belgium, Canada, Denmark, Germany, France, Hungary, Ireland, Norway, Poland, Spain, Sweden, Switzerland, UK, and the United States) review their course modules annually to ensure that they adhere to latest international standards and best practice. Although all MSAG members are also OSCE members, recipients of MSAG assistance need not be members of that organization. Officials from some 30 countries in the OSCE 'region' as well as Africa have participated in MSAG-sponsored courses at regional training centres (e.g. RACVIAC in Croatia, International Peace Support Training Centre in Kenya, and NATO School in Germany, and at MSAG members' training facilities. Countries receiving direct and sustained support to manage their weapons and munitions stores include—but are not limited to—Bosnia and Herzegovina, Ethiopia, Moldova, Tajikistan, and Turkmenistan.

PUBLICATIONS AND MATERIALS OF NOTE
■ MSAG, 2013. *Coursebook on Physical Security and Stockpile Management of Arms, Ammunition and Explosives.*

* Wasifu huu, pamoja na nyingine 36 katika Kijitabu, hautumiki kama msimamo au hati rasmi ya mhusika aliye kwenye wasifu.

Kuhusu Small Arms Survey

Ni kituo cha ubora duniani ambacho madhumuni yake ni kutoa taarifa adilifu, yenye ushahidi na inayohusu sera kuhusu vigezo vyote vya silaha ndogo ndogo na vita vya silaha. Ni chanzo muhimu cha kimataifa cha kutoa taarifa, utaalamu na uchambuzi wa masuala ya silaha ndogo ndogo na vita vya silaha. Utenda kama rasilimali kwa serikali, watengeneza sera, watafiti na asasi za kiraia. Makao makuu yake yapo Geneva, Uswisi katika taasisi ya elimu ya juu ya masomo ya Kimataifa na Maendeleo.

Small Arms Survey ina wafanyakazi wa kimataifa wenye ujuzi wa mafunzo ya ulinzi na usalama, sayansi ya kisiasa, sheria, uchumi, masomo ya maendeleo, sosholojia na elimu ya jinai pamoja na ushirikiano na mtandao wa watafiti, taasisi za wabia, mashirika yasiyo ya kiserikali na serikali katika nchi zaidi ya 50.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti ya www.smallarmssurvey.org.

Mara ya kwanza kuchapishwa kwa lugha ya Kiingereza: Aprili 2014

Toleo hili katika lugha ya Kiswahili: Septemba 2015

Sifa

Waandishi: Eric G. Berman, Benjamin King, na Pilar Reina

Wahariri: Nsia Humphrey Shoo (humphreynsia@gmail.com) na Nivoneia Yonazi Kikaho

Muundo na mpangilio: Rick Jones (rick@studioexile.com)

Maelezo ya mawasiliano

Small Arms Survey
Maison de la Paix
Chemin Eugène-Rigot 2E
CP 136 – 1211 Geneva
Switzerland

simu +41 22 908 5777
faksi +41 22 732 2738
info@smallarmssurvey.org
www.smallarmssurvey.org

Umefadhiliwa na Office of Weapons Removal and Abatement (PM/WRA)



Uchapishaji huu unaunga mkono Programu ya SaferGuard ya Umoja wa Mataifa

